



WIZARA YA ARDHI, NYUMBA  
NA MAENDELEO YA MAKAZI

# Jarida la mtandaoni

BODI YA  
UHARIRI

MARY MAKONDO  
Mwenyekiti

LUSAOJO MWAKABUKU  
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha  
Mawasiliano Serikalini

WAANDISHI

Munir Shemweta   Eliafile Solla  
Hassan Mabuye   Magreth Lyimo



Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi akimkabidhi Hati ya kiwanja cha jengo la Bunge Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Ndugai

## WIZARA YA ARDHI YAKABIDHI HATI YA KIWANJA CHA JENGO LA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

### Na Lusajo Mwakabuku

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi amemkabidhi hati ya kiwanja cha jengo la bunge Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Ndugai.

Wakati wa kukabidhi hati hiyo Mhe. Lukuvi alimshukuru Mhe. Spika kwa kutilia mkazo maagizo ya Serikali kwa taasisi zake ya kupima na kuchukua hati zao ili kuyalinda maeneo yao na kuepusha migogoro na wananchi.

Mhe. Lukuvi pia ametumia nafasi hiyo kuzitaka taasisi nyingine za Serikali kuhakikisha zinapima na kuchukua hati za maeneo wanayoyamiliki. Upimaji huo unaweza kufanywa na wapima wa serikali au wapima binafsi ambaeo wamesajiliwa na Wizara ya Ardhi.

Akiipokea hati hiyo katika tukio hilo lilioshuhudiwa na Katibu wa Bunge Nd. Stephen Kagaigai, Spika wa Bunge Mhe. Job Ndugai (Mb) alisema kwamba sasa badala ya kuwa wapita njia na wapangaji, kwa hati walizokabidhiwa anaamini sasa wapo nyumbani.

*"Nami nitoe wito kwa Taasisi zote za kiserikali Wizara na Mashirika kuhakikisha kwamba maeneo yao yote yamepimwa na yana hati"*

Alisema Spika Ndugai.

Akigeukia upande wa wananchi katika umiliki wa ardhi, Mhe. Waziri Lukuvi amewataka wale ambao maeneo yao hayajarasimishwa wafanye hivyo kulinda milki zao na wale wanaomiliki kisheria wahakikishe wanalipa kodi zao kwa wakati kuepusha usumbufu utakaotokana na limbikizo la kodi hizo.

Wizara ya ardhi itaendelea kutoa ushirikiano kupitia Ofisi zake zilizoanzishwa kila mkoa ili kurahisisha upimaji na upatikanaji wa hati kwa taasisi za serikali na jamii yote kwa ujumla.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Ndugai akioneshesha Hati za viwanja vya majengo ya Bunge baada ya kukabidhiwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi.

# DAR YAWEKA MKAKATI KUKAMILISHA ZOEZI LA URASIMISHAJI



Mratibu wa zoezi wa Urasimishaji Makazi Holela Paul Kitosi

## Na. Munir Shemweta

**K**atika kuhakikisha kazi ya urasimishaji makazi holela inakamilika, ofisi ya kamishna wa ardhi Msaidizi mkoa wa Dar es Salaam imojiwekea mikakati ya kukamilisha zoezi hilo haraka na kumilikisha wananchi maeneo yao.

Mikakati hiyo ni pamoja na kanzi data ya kujua kila kinachofanyika kwenye mitaa ambayo zoezi la urasimishaji linafanyika na sasa ofisi ya ardhi mkoa inajua viwanja, michoro ya mipango miji pamoja na idadi ya maombi ya hati zilizotolewa kwenye maeneo husika. Akielezea mikakati hiyo Mratibu wa zoezi la Urasimishaji Makazi Paul Kitosi alisema, 'Kanzi data hiyo mbali na mambo mengine inasaidia kufuatilia mkakati mzima wa urasimishaji kwenye mitaa ya halmashauri za manipaa ya mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha, Kitosi ambaye pia ni Mtaalamu wa Mipango Miji alisema, katika jitihada zake ofisi ya ardhi mkoa wa Dar es Salaam imekuwa ikifanya mikutano ya mara kwa mara na wadau yakiwemo Makampuni ya Upangaji, Upimaji sambamba na kuwa na mawasiliano na Kamati za Wananchi katika mkoa mzima na kusisitiza kuwa hatua hiyo imesaidia kujua changamoto.

Kwa upande wake Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Dar es Salaam Idrisa Kayera alisema, kazi za urasimisaji makazi katika mkoa wake zinaendelea ingawa aliweka wazi kuwa bado kuna changamoto kadhaa zinazosababisha zoezi kutokamalika kwa haraka.

Aliitaja changamoto moja kuwa ni baadhi ya Kampuni kutofanya vizuri ambapo hata hivyo alieleza kuwa tayari wizara yake ilianza kuchukua hatua kuhakikisha Makampuni yasiyofanya vizuri yanachukuliwa hatua za kisheria.

"Hatua zilizoanza kuchukuliwa ni pamoja na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi kukutana na makampuni yanyohusika na zoezi hilo sambamba Katibu Mkuu wa Wizara kuelekeza makampuni yaliyoshindwa kukamilisha kazi kwa wakati kuchukuliwa hatua" alisema Kayera.

Kwa mujibu wa Kamishna huyo wa ardhi Msaidizi mkoa wa Dar es Salaam, pia bodi ya Upimaji imeshachukua hatua ya kusimamisha kampuni zisizokamilisha kazi kwa wakati sambamba na makampuni ya mipango miji kusimamishwa kuchukua kazi nyingine.

Hata hivyo, Kayera alisema kumekuwa na matokeo chanya kwa baadhi ya kampuni ambazo zimeanza kutekeleza na juhudu zinaendelea ili kazi ikamilike.

**"Ofisi ya ardhi mkoa imeziwekea mikakati Mamlaka za Upangaji, Wataalamu wa Ardhi, Mipango Miji, Wapimaji na Wasimamizi wa Ardhi katika halmashauri za manipaa kuhakikisha zoezi linaenda vuzuri na kupatiwa taarifa zote za viwanja vilivyopimwa katika kila mtaa, kila afisa amepewa mtaa wa kufuatilia zoezi hilo"** alisema Kitosi.



Mratibu wa zoezi la urasimishaji katika eneo la Kivule Dar es Salaam Kutoka Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) Manyama Majogolo akizungumza na wananchi wa eneo hilo wakati wa zoezi la urasimishaji.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline Mabula akiongea na wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi (hawa-pichani) na kutoa ufanuzi wa msamaha wa kodi kwa taasisi za dini.

## NAIBU WAZIRI WA ARDHI AWAONYA WANAO TUMIA VIONGOZI KUKWEPA KULIPA KODI SINGIDA

### Na Lusajo Mwakabuku

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mh. Angeline Mabula amefanya ziara ya siku moja Mkoani Singida kwa lengo la kukukutana na wadaiwa wenye madeni ya muda mrefu (wadaiwa sugu), kujadili changamoto zao na kutafuta suluhisho kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria dhidi yao.

Naibu Waziri Mabula amechukua hatua hiyo ikiwa ni sehemu ya ziara zake katika mikoa mbalimbali nchini kufuatilia makusanyo ya kodi ya pango la ardhi pamoja na kutatua



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline Mabula akiona katika picha ya pamoja na watumishi wa ofisi ya Ardhi ya Mkoani Singida mara baada ya kumaliza Ziara yake mkoani humu.

changamoto zake. Awali wakati akipata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mkoa, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoan wa Singida Shamim Hoza pamoja na timu yake walimueleza Naibu Waziri kuwa kumekuwepo na changamoto ya baadhi ya wadaiwa "kukingiwa kifua" na viongozi.

**"Lengo la kuja hapa kuongea na ninyi leo ni kujua hii sintofahamu juu ya ulipaji kodi, kumekuwa na changamoto za ulipaji ambapo watumishi wetu wamekuwa wakikwamishwa na baadhi ya wamiliki kukimbilia kwa viongozi ili wawatetee wasilipe kodi, naomba niwakumbushe kwamba, wanachelewesha tu lakini kodi ya serikali ni lazima ilipwe. Ningombwa kwa upande wa viongozi kuanzia Wizara, Mkoan wa Wilaya tufanye kazi kama timu katika kuhakikisha kodi inakusanywa badala ya kukwamisha"** Alisema Naibu Waziri.

Moja kati ya makundi ambayo yalijitetea kushindwa kulipa kodi kwa wakati ni pamoja na taasisi za dini zilizojitetea kuwa hazijijendeshi kwa faida na kwamba zingeomba kupata msamaha wa kodi. Pia kundi hilo lilihitaji ufanuzi kutoka kwa Naibu Waziri kwa maelezo kwamba serikali ilitoa msamaha wa kodi mwaka 2018 kwa asasi za huduma zisizojendesa kwa kutengeneza faida.

Akilieleza kwa kina suala hilo, Naibu Waziri Mabula alisema, kwa madhehebu ya dini msamaha wa kodi ya ardhi umetolewa ktk maeneo yalipojengwa majengo ya kuabudia yaani kanisa, au msikiti. Aidha nilieleza msamaha huo ni lazima uombwe, wahusika wanatakiwa kuomba kwa kujaza fomu maalumu na wawanatakiwa pia kufanya mgawanyo kama kuna



Baadhi ya wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi wakimsikiliza Mh.Dkt. Angeline Mabula. Naibu Waziri wa Ardhi alipofika mkoani Singida kuzungumza nao.

huduma zingine ndani ya kiwanja kimoja.

"Niweke wazi kwamba kama wewe unaendesha kanisa, serikali imetoa msamaha eneo ambalo kumejengwa sehemu ya kuabudia tu. Iwe kanisa au msikiti, ila pale utakapoendeleza kujenga majengo mengine kwenye ardhi hiyo hiyo kwa ajili ya kutoa huduma zingine ambazo mtawalipisha wananchi kama vile shule, hospitali na vitu kama hivyo basi ni lazima eneo hilo lilipiwe kodi. Ila kama unatoa huduma hizo bure kabisa uje kwa Kamishna utajaza fomu maalumu na akijiridhisha hapo utaombewa msamaha kwa huduma hiyo" Aliongeza Naibu Waziri.

Wakati huo huo, Naibu Waziri ameliagiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha linawapitia wapangaji wote Mkoani Singida na kujiridhisha kuwa ni wapangaji halali. Hii inatokana na kujitokeza kwa hali ya wapangaji walio na mikataba na NHC kupangisha watu wengine. Zoezi hili tayari limeshafanyika Dar es salaam ambapo wapangaji walioikutwa wamepanga kupitia wapangaji wenye mikataba na Shirika la Nyumba la Taifa waliondolewa au kupewa mikataba kama wapangaji halali wa nyumba hizo.

Singida ni moja ya Mikoa yenyen madeni sugu yanayohusisha wafanyakibashara, asasi zisizo za kiserikali pamoja na Taasisi za Serikali ambapo hadi kufikia tarehe 15 Aprili mwaka huu Ofisi ya Kamishna Msaidizi Mkoan wa Singida kwa kushirikiana na Halmashauri za manispaa ilisambaza hati za madai 679 zenye thamani ya zaidi ya bilioni 1.3 ambapo kati ya hati hizo wadaiwa 213 wanaodaiwa wameshafikishwa katika mahakama za Mabaraza ya Ardhi.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline Mabula akipata maelezo kuhusu nyumba zinazopangishwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).



Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobel (kushoto) akipata maelezo kuhusiana na kifaa cha upimaji kutoka kwa mwananfunzi wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) wakati wa mahafali ya 39 ya chuo hicho.

# MAHAFALI ARIMO

KATIBUTAWALAMKOAWAMOROGORO  
AAGIZA HALMASHAURI KUSHIRIKIANA  
NA CHUO CHA ARDHI MOROGORO  
KUMALIZA MIGOGORO YA ARDHI

Na Eliafile Solla

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobel amemuagiza Mkuu wa chuo cha Ardhi Morogoro kuandika barua kwenda Halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro kuona jinsi gani wanaweza kuwatumia wataalam kutoka chuoni hapo kumaliza migogoro ya ardhi inayosababishwa na ujenzi holela na kugombania mipaka ya maeneo.



Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) Huruma Lugala akisoma hotuba yake wakati wa mahafali ya 39 ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

Kalobel ameyasema hayo wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenye sherehe za mahafali ya 39 ya Chuo cha ardhi Morogoro ambapo jumla ya wahitimu 394 walitunukiwa vyeti na kati yao 110 walikuwa wa kike, 284 wa kiume na kauli mbii ya sherehe hizo ilikuwa ni "Usimamizi bora wa rasilimali za ardhi ni msingi wa maendeleo endelevu na jumuishi".



Sehemu ya wahitimu wa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO)

**"Ni aibu kwa Mkoa wa Morogoro kuendelea kuteseka na Migogoro ya ardhi wakati Chuo kinachozalisha watalaam wa Kupanga na Kupima kipo hapa hapa. Naagiza kabla mwaka huu haujaisha Halmashauri zote za mkoa wa Morogoro ziwe na mpango mkakati kuona jinsi gani ya kushirikiana na Chuo cha Ardhi Morogoro kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa"** alisema Kalobel.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro Bwn. Huruma Lugala alisema, chuo kinao usajili kamili (Full Registration) pamoja na ithibati kamili (Full accreditation) ya Baraza la Taifa la Elimu na Ufundu yaani 'NACTE'. Usajili huo na ithibati vinatoa uwezo kwa chuo kujipanua kwa kuanzisha kozi mbalimbali zenyne tija kwa Taifa na jamii kwa ujumla.

Mbali na kuzalisha wataalam wa Kupanga na Kupima, Chuo cha ardhi Morogoro kimekuwa kikishiriki kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu na kufanya miradi ya urasimishaji ambayo hadi sasa inatekelezwa katika Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Morogoro, Mtwara, Kilimanjaro na Iringa.

# MATUKIO KATIKA PICHA



01

Vifaa vya upimaji



02

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe William Lukuvi akitatua migogoro ya ardhi katika eneo la Bunju Manispaa ya Kinondoni Dar es Slaam.



Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe William Lukuvi akizungumza na wananchi wa Mabwepande Manispaa ya Kinondoni, Dar es Slaam wakati wa kusuluhisha mgogoro katika eneo hilo.



03




04



05

Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Denis Masami akifafanua jambo wakati zoezi la uhamasishaji ulipaji wa kodi ya pango la ardhi katika eneo la Mkonze mkoani Dodoama.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe Dkt. Angeline Mabula akioneshwa eneo lenye mgogoro katika kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza na Mkuu wa wilaya ya Ukerewe Kanali Lucas Magembe.



06

Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe Dkt Angeline Mabula akioneshwa eneo la uwekezaji katika wilaya ya Mkinga mkoani Tanga na Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Dkt Yona Maki.